WIZARA YA NISHATI


# MALAGARASI

# MW 49.5

Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia maji wa Malagarasi

Eneo: Kigoma






## KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2023/24

- Mkandarasi Dongfung Electric International Corporation wa ujenzi wa bwawa anaendelea na kazi za awali toka tarehe 30.4.2024 kuanza ujenzi wa bwawa;

- Kazi ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 kutoka kwenye bwawa la kuzalisha umeme hadi katika kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe zinaendelea kwa Mkandarasi Shyama Power India Limited na hadi sasa mradi upo asilimia 31, na kukamilisha ununuzi wa Kandarasi ya kusambaza na kuunganisha wateja watakaopitiwa na mradi wa msongo wa kV132 unaendelea.











## UTEKELEZAJI WA MRADI HADI MWEZI JUNI 2024

### UJENZI WA BWAWA

» Mkandarasi wa ujenzi wa Bwawa kampuni ya Dongfang anaendelea na kazi za awali ikiwemo ukamilishaji wa kwanza wa Ubunifu wa mradi (Level 1 Design), ukusanyaji wa mitambo ya ujenzi (Mobilization) kwenye eneo la mradi, ujenzi wa barabara ya kuelekea eneo la mradi hatua ya awali pamoja na utafiti wa awali wa eneo la mradi (Detailed/Topographic survey). Kwa sasa utekelezaji umefikia asilimia 2.22.

## UJENZI WA NJIA KUU YA KUSAFIRISHA UMEME (132kV)

- Mkandarasi wa ujenzi wa Njia kuu ya kusafirisha Umeme msongo wa kilovoti 132 kampuni ya Shyama Power India anaendelea na kazi za ujenzi wa misingi ya Nguzo za umeme (Tower Foundations) tokea tarehe 19.06.2024 pamoja na utengenezaji na usimikaji wa mipaka ya njia ya umeme (Installation of Wayleave concrete marker). Usafirishaji wa vifaa vya mradi unaendelea kwa vifaa vyote vilivyofanyiwa ukaguzi (FAT). Kwa sasa utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 31.44.

## UJENZI WA MTANDAO WA USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI

- Zoezi la tathmini ya Zabuni (Bids Evaluation) linaendelea ambapo jumla ya zabuni 14 zilipokelewa kwa Lot 1 na zabuni 13 kwa Lot 2. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa 7 mwaka 2024